

## **VIDOKEZO KUHUSIANA NA MATUMIZI BORA YA NYWILA.**

Nywila ni neno la siri linalotumiwa kumtambulisha mtu na kumpa ruhusu ya kutumia mfumo fulani.

Taasisi moja itwayo Ponemon ilitoa takwimu zifuatazo:

1. 51% ya watu hutumia nywila moja katika akaunti 5 za biashara na za kibinafsi.
2. 69% ya watu huwapa nywila zao na watu wao wa karibu
3. 57% ya waliohojiwa ambao wamepata shambulio la ulaghai (Phishing Attack) hawakubadilisha tabia zao za nywila.

Mambo yafuatayo yatakusaidia wewe mtumiaji wa kawaida ama kwa kampuni/taasisi kuhakikisha nywila ya mtumiaji ipo salama dhidi ya shambulio;-

### **Mtu Binafsi:**

1. Hakikisha nywila yako ni siri na unaifahamu wewe tu na sio mtu mwingine.
2. Hakikisha nywila yako inachukua herufi (character) kuanzia nane.
3. Hakikisha nywila yako inachukua herufi, herufi maalum na namba, herufi ndogo na herufi Kubwa pia. Mfano: TaNz@n!@01.
4. Hakikisha nywila yako sio neno la kutabirika.
5. Hakikisha nywila yako una ibadilisha kwa wakati maalum. Angalau baada ya miezi mitatu badilisha nywila yako.
6. Hakikisha nywila yako moja huitumii katika mifumo mingine.
7. Usiamini program yako tumishi (browser) kutunza nywila zako. Usitunze nywila zako humu.

**KAMPUNI/SHIRIKA/TAASISI:**

1. Hakikisha kuna sera inayomtaka kila mtumiaji wa mfumo anapaswa kuwa na nywila yake ili kumuwezesha kutumia mifumo fulani.
2. Hakikisha mtumiaji wa mfumo fulani analazimishwa kubadilisha nywila yake kwa mara ya kwanza kuingia katika mfumo fulani ama nywila ikimalizika kutumika (Password expired).
3. Hakikisha password hutuzwa kwa katika mfumo usio eleweka kwa mtumiaji (Password encryption) na mahali panapotunzwa asiwezi fika mtumiaji wa kawaida wa mfumo huo.
4. Hakikisha mfumo utakaotumika kunyumbulisha password (Password encryption Algorithm) usiwe wa kawaida wa kumfanya mharifu kufanya shambulio kwa haraka na wepesi.
5. Hakikisha kuna sera inayo mtaka mtumiaji kuhakikisha anatengeneza/chagua nywila yenye sifa zakuwa nywila imara yaani imehusisha sifa zote za kuunda nywila imara, mfano isiwe chini ya herufi 8, iwe na mchanganyiko wa herufi kubwa, helufi ndogo na herufi maalum na namba.
6. Hakikisha mfumo una uwezo wa kukataa nywila zinazojulikana ambazo zinamfanya mhalifu kubashiri nywila ya mtumiaji.
7. Hakikisha mtumiaji wakati anaingiza nywila yake isiwe inaonekana ama kusomeka bali iwe imefichwa.
8. Hakikisha mfumo umlazimishwe mtumiaji kubadilisha nywila yake angalau baada ya siku 90 kutengenezwa.
9. Hakikisha mfumo uwe na uwezo wa kutambua ni mara ngapi mtumiaji ameingiza nywila kwa kukosea. Na kama ikizidi angalau mara 5 basi akaunti ya mtumiaji huyo ifungwe.
10. Hakikisha kuwepo na mfumo wa kufanya majaribio kwa kila akaunti juu ya nywila dhaifu (Password Attack) na kuzifunga.

**Imeandaliwa na:**

Cyberjamii Organization

March, 2020

***Be aware. Be secure!***